Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430

AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**EDISON SIMON MWOMBEKI DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI NA. 030/2018**

**HUKUMU KUHUSU UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, tarehe 13 Novemba 2024**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama), imetoa hukumu katika kesi ya *Edison Simon Mwombeki dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

Edison Simon Mwombeki (Mleta Maombi) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Maombi). Wakati wa kuwasilisha Maombi haya, alikuwa amefungwa katika Gereza Kuu la Butimba jijini Mwanza, baada ya kusikilizwa kesi, akapatikana na hatia, na kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 kwa kosa la ubakaji. Mleta Maombi alidai haki zake zilikiukwa wakati wa kuendeshwa kesi mbele ya mahakama za kitaifa.

Kuhusiana na mamlaka ya kisheria, Mjibu Maombi alipinga mamlaka halisi ya Mahakama na kudai kwamba haijapewa mamlaka ya rufaa ya "kumtoa gerezani Mleta Maombi". Mjibu Maombi aliendelea kusema kwamba Mleta Maombi alikuwa hajashtaki ukiukwaji wowote wa haki za binadamu ambao alidai alikuwa amefanyiwa. Badala yake, alitaja tu ukweli kwamba haki zake zilikiukwa lakini alishindwa kuonyesha jinsi ukiukaji huo ulivyofnyika.

Kuhusiana na hoja kwamba Mahakama itakuwa inatekeleza mamlaka ya mahakama ya rufaa, Mahakama ilisisitiza msimamo wake kwamba haitekelezi mamlaka ya mahakama ya rufaa kuhusiana na madai ambayo tayari yamechunguzwa na mahakama za kitaifa. Hata hivyo, wakati huohuo, licha ya kwamba Mahakama si mahakama ya rufaa dhidi ya mahakama za ndani, bado ina uwezo wa kutathmini usahihi wa kesi za ndani endapo zimefanywa kinyume cha viwango vilivyowekwa katika vyombo vya kimataifa vya haki za binadamu vilivyoidhinishwa na Serikali inayohusika. Katika kutekeleza kazi iliyotajwa hapo juu, Mahakama kwa kufanya hivyo haitakuwa mahakama ya rufaa.

Kuhusu madai ya Mjibu Maombi kwamba Mahakama haikuwa na mamlaka ya kutoa amri ya kuachiliwa huru, Mahakama ilirejelea Kifungu cha 27(1) cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki) kinachosema

kwamba "[ikiwa Mahakama itabaini kuwa kumekuwa na ukiukaji wa haki za binadamu au za watu, itatoa amri zinazofaa ili kusuluhisha ukiukaji huo, ikiwa ni pamoja na malipo mazuri ya fidia." Kwa hivyo, Mahakama ilihitimisha kwamba ina mamlaka ya kutoa aina tofauti za fidia, ikiwa ni pamoja na kuachiliwa huru kutoka gerezani, ili mradi ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulihitaji amri kama hiyo itolewe. Kwa sababu hizi, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi lililotolewa na Mjibu Maombi.

Mahakama ilibainisha pia kwamba kulingana na kwamba ukiukaji unaodaiwa kufanywa uliwasilishwa mbele yake unahusu haki zilizowekwa katika Mkataba, ambao Mjibu Maombi ni Mhusika, ilikuwa na mamlaka muhimu ya kuchunguza Maombi haya.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka yake havikupingwa na Mjibu Maombi, hata hivyo, Mahakama ilivichunguza. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka binafsi kwani, tarehe 29 Machi 2010, Mjibu Maombi iliweka Azimio lililotolewa chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki, ambacho kinaruhusu watu binafsi kuwasilisha maombi dhidi ya Mjibu Maombi kulingana na Kifungu cha 5(3) cha Itifaki. Mahakama ilisisitiza kwamba Mjibu Maombi kuondoa Azimio hilo, mnamo tarehe 21 Novemba 2019, hakukuathiri Maombi haya kwani uondoaji huo ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 22 Novemba 2020, ambayo ilikuwa tarehe baada ya Maombi haya kuwasilishwa, mnamo tarehe 1 Novemba 2018.

Mahakama pia iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa ulitokea baada ya Mjibu Maombi kuwa mhusika wa Itifaki. Mwisho, ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo, ikizingatiwa kuwa ukweli wa jambo hilo ulitokea ndani ya eneo la Mleta Maombi.

Mahakama iliona kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Itifaki, lazima iamue kuhusu ukubalifu wa kesi zilizowasilishwa mbele yake. Katika suala hili, Mjibu Maombi aliibua pingamizi la jumla kuhusu Maombi, kwa kudai kwamba hayakukidhi mahitaji ya ukubalifu. Hata hivyo, haikuthibitisha pingamizi lake wala haikubainisha pingamizi hilo linaelekezwa kwenye matakwa yapi ya ukubalifu. Hata hivyo, Mahakama ilitathmini vigezo vyote vya ukubalifu ili kuhakikisha kwamba Maombi yalitimiza viwango vinavyohitajika.

Kwa hivyo, Mahakama ilibainisha kuwa Mleta Maombi alikuwa ametambuliwa kwa udhahiri kwa jina katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni za Mahakama. Iliona pia kwamba madai ya Mleta Maombi yalilenga kulinda haki zake kulingana na Kifungu cha 3(h) cha malengo ya Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo Maombi yalizingatia Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni za Mahakama.

Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430



Aidha, Mahakama ilibaini kwamba lugha iliyotumika katika Maombi haikuwa ya dharau au ya matusi kwa Mjibu Maombi au taasisi zake katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni za Mahakama. Maombi haya pia hayakutoka tu na habari zinazosambazwa kupitia vyombo vya habari kwani yalitokana na nyaraka za mahakama kutoka mahakama za ndani za Mjibu Maombi katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni za Mahakama. Mahakama pia iliona kwamba Maombi yalikuwa yamewasilishwa kwenye Mahakama baada ya kumaliza taratibu za ndani za Mjibu Maombi. Mahakama ilibainisha kuwa Mleta Maombi alikata rufaa hadi Mahakama ya Rufaa, chombo cha juu cha mahakama cha Mjibu Maombi, na rufaa hiyo iliamuliwa wakati Mahakama hiyo ilipotoa hukumu yake mnamo tarehe 18 Oktoba 2016, kwa kutimiza Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama.

Kuhusiana na sharti la Maombi kuwasilishwa ndani ya wakati unaofaa, Mahakama ilibainisha kuwa uamuzi wa mwisho wa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ulitolewa tarehe 18 Oktoba 2016 na Mleta Maombi aliwasilisha Maombi yake mbele ya Mahakama hii tarehe 1 Novemba 2018. Mahakama iliona kwamba kipindi cha miaka miwili na siku 14 kilichopita kabla ya kuwasilisha Maombi yake mbele ya Mahakama hii ulikuwa ni muda unaofaa katika mazingira haya, ikizingatiwa, miongoni mwa mambo mengine, kwamba Mleta Maombi amefungwa, si mwanasheria na anajiwakilisha, na kwa hivyo, iliona kwamba masharti ya Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama yametimizwa.

Mwisho, Mahakama ilibaini kuwa kesi hiyo haikuwa imeshughulikiwa hapo awali mbele ya mahakama nyingine ya kimataifa na kwa hivyo ilizingatia Kanuni ya 50(2)(g) ya Kanuni za Mahakama. Kwa hivyo, Mahakama ilihitimisha kwamba Maombi haya yalikuwa yanakubalika na ilitupilia mbali pingamizi la jumla la Mjibu Maombi kuhusu ukubalifu wa Maombi haya.

Kuhusu uzingatiaji wa sheria, Mahakama iliangalia endapo Mjibu Maombi alikiuka haki za Mleta Maombi. Kwa kuzingatia mawasilisho ya Mleta Maombi, Mahakama iliona kwamba suala kuu katika Maombi haya ni madai ya ukiukaji wa haki ya Mleta Maombi ya kusikilizwa kwa haki, inayolindwa chini ya Kifungu cha 7(1) cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba), ingawa Mleta Maombi hakurejelea wazi kifungu hiki cha Mkataba. Kwa hivyo, Mahakama iliangalia madai haya kwanza, kabla ya kutathmini madai ya ukiukaji wa Kifungu cha 3(2) na 5 cha Mkataba.

Mleta Maombi alidai kwamba (i) mahakama zilizoendesha kesi na mahakama ya rufaa zilikosea katika sheria na ukweli kwa kumhukumu kwa kuzingatia ushahidi wenye mashaka na usio na mashiko wa shahidi mmoja, pamoja na shuhuda zinazojipinga zisizo na uthabiti, na kwamba (ii) mahakama zilizoendesha kesi na mahakama ya rufaa zilishindwa kuzingatia vya kutosha ushahidi uliowasilishwa katika utetezi wake.

Kuhusiana na madai ya kwanza, Mahakama ilitupilia mbali madai ya Mleta Maombi na ikaona kwamba Mjibu Maombi hakukikuka haki yake ya kusikilizwa, inayolindwa chini ya Kifungu cha 7(1) cha Mkataba, baada ya kuona kwamba namna ambavyo kesi zilishughulikiwa mbele ya mahakama za ndani haikuonesha makosa dhahiri yanayohitaji uingiliaji kati wa Mahakama hii. Kuhusiana na madai ya pili, Mahakama ilibaini kwamba Mleta Maombi hakutoa mawasilisho mahususi au kutoa ushahidi kuthibitisha kwamba namna ambavyo kesi zilishughulikiwa mbele ya mahakama za ndani kuhusiana na kuzingatia ushahidi katika utetezi wake ilisababisha upotoshaji wowote mkubwa wa haki au ilisababisha ukiukwaji wa haki ya kusikilizwa ya Mleta Maombi. Kwa kuzingatia hili, Mahakama iligundua kwamba Mjibu Maombi hakukikuka haki ya Mleta Maombi ya kusikilizwa, inayolindwa chini ya Kifungu cha 7(1) cha Mkataba.

Mahakama ilibainisha pia kwamba Mleta Maombi hakuwa ametoa maoni yoyote mahususi wala kutoa ushahidi kwamba Mjibu Maombi alikiuka haki zake za ulinzi sawa mbele ya sheria, na utu inayolindwa chini ya Kifungu cha 3(2) na 5 cha Mkataba, mtawalia. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba hakuna msingi wa kuona ukiukaji na iliona kwamba Mjibu Maombi hakukiuka Kifungu cha 3(2) na 5 cha Mkataba.

Baada ya kuona kuwa Mjibu Maombi hakuwa amekiuka haki yoyote ya Mleta Maombi, Mahakama ilitupilia mbali maombi ya Mleta Maombi ya kupewa fidia.

Kuhusu gharama, Mahakama iliamua kwamba kila upande unapaswa kubeba gharama zake.

**Maelezo zaidi**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama, inaweza kupatikana kwenye tovuti kwenye: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0302018

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*